# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA KILICHOFANYIKA TAREHE 20 MACHI,2022 KATIKA OFISI YA KITENGO CHA MANUNUZI

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

| | |
|---|---|
| 1. Kamili F Makiya | M/Kiti |
| 2.Michael Mapela | Katibu |
| 3.Uria Y, Ndelwa | Mjumbe |
| 4. Rose J Kitundu | Mjumbe |
| 5. Prosister Tairo | Mjumbe |
| 6. Jofrey E. Pima | Mwanasheria |

**WASIO HUDHURIA**

| | |
|---|---|
| 1. Mohamed Semdoe | Kwa taarifa |

**SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1.Rehema Ndaga | Sekretarieti |

**WAALIKWA**

| | |
|---|---|
| 1.Johnson Limbe | Meneja mradi ujenzi wa jengo la Halmashauri |

**AGENDA ZA KIKAO**

1.Kufungua kikao.

2.Kuridhia agenda.

3. Kupokea na kuridhia maombi ya kutumia njia ya manunuzi ya Force Account kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya wilaya,zahanati, shule za msingi na sekondari fedha kutoka serikali kuu.

4.Kufunga kikao.

**AGENDA Na BYZ. 03,2021/2022/01-KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 10.09 jioni kwa kuwakaribisha na kuwashukuru wajumbe waliohudhuria kikao hicho.

**AGENDA Na BYZ. 03,2021/2022/02 -KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Katibu aliwasomea wajumbe agenda za kikao, Baada ya zoezi hilo kufanyika wajumbe waliridhia agenda hizo zijadiliwe.



CamScanner

**AGENDA NA.BYZ .03,2021/2022/03- KUPOKEA NA KURIDHIA MAOMBI YA KUTUMIA NJIA YA SINGLE SOURCE KWA AJILI YA KUTEKELEZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA AFYA,SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU**

qwe

Afisa elimu sekondari aliwasomea wajumbe wa kikao mchanganuo wa fedha iliyotolewa na serikali kuu kwa ajili miundombinu ya shule za msingi na sekondari mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

**IDARA YA ELIMU MSINGI:-**

Katika idara ya elimu msingi imepata mgao wa fedha kiasi cha shilingi 580,000,000.00 Fedha hizo zitatumika kujenga vyumba vya madarasa 29 katika shule zifuatazo:- Shule shikzi za Masimba ujenzi wa madarasa 5 ,Toroma ujenzi wa madarasa 4 ,Muungano ujenzi wa madarasa 3,Majengo ujenzi wa madarasa 3,Majengo Mapya, ujenzi wa madarasa 2. Kaloleni ujenzi wa madarasa 2.,Walimbe ujenzi wa madarasa 2,Lugoba ujenzi wa madarasa 2,Pampai ujenzi wa madarasa 2.,Magandi ujenzi wa madarasa 2,Mangasta ujenzi wa madarasa 2 . Katika mwongozo kila darasa linatakiwa kukamilika kwa gharama ya shilingi 20,000,000.00 tu.

**IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

Idara ya elimu sekondari imepata mgao wa fedha kiasi cha shilingi 1,300,000,000.00 Fedha hizo zitatumika kujenga vyumba vya madarasa 65 katika shule zifuatazo:- Shule ya sekondari Soya ujenzi wa vyumba vya madarasa 3,. Shule ya sekondari Songolo ujenzi wa chumba darasa 1 Shule ya sekondari Sanzawa ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 Shule ya sekondari Paranga ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,Shule ya sekondari Kelema balai ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, Shule ya sekondari Msakwalo ujenzi wa vyumba vya madarasa 5, Shule ya sekondari Msaada ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, Shule ya sekondari Mrijo ujenzi wa vyumba vya madarasa 6, Shule ya sekondari Mpendo ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 Shule ya sekondari Mondo ujenzi wa vyumba vya madarasa 5, Shule ya sekondari Makorongo ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, Shule ya sekondari Lalta ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 Shule ya sekondari Kwamtoro ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, Shule ya sekondari Kimaha ujenzi wa vyumba vya madarasa 5, Shule ya sekondari Jangalo ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 Shule ya sekondari Itolwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 5, Shule ya sekondari Gwandi ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 Shule ya sekondari Goima ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, Shule ya sekondari Farkwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 2, na Shule ya sekondari Dalai ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 na Shule ya sekondari Chemba ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 Pia katika mwongozo kila darasa linatakiwa kukamilika kwa gharama isiozidi shilingi za kitanzania 20,000,000.00 tu.



CamScanner

**IDARA YA AFYA**

Katika idara ya Afya fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ifuatavyo:-

Ujenzi wa miundombinu katika Hospitali ya wilaya kiasi cha Tsh,800,000,000.00,ukamilishaji wa Zahanati ya Chemba shilingi 50,000,000.00,ujenzi wa jengo zahanati ya Wairo shilingi 50,000,000.00 na ujenzi wa jengo jipya zahanati ya jangalo shilingi 50,000,000.00

***Mjadala/Azimio***

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kwa kina.baada ya mjadala Wajumbe waliridhia kutumia njia ya manunuzi ya forcé Account katika ujenzi huo. ,Njia hiyo ya manunuzi itarahisisha kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na nguvu kazi ya jamii itatumika.

Hivyo wajumbe waliagiza kuwa mchakato wa kuwapata mafundi ufanyike haraka iwezekanavyo.

**AGENDA Na BYZ. 01,2021/2022/10 -KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti wa kikao aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano wao katika kujadili na kutoa maamuzi,mwenyekiti alikifunga kikao mnamo Saa 8.10 jioni

**UMETHIBITISHWA NA;**

....................................      ....................................

**KATIBU**      **MWENYEKITI**

**TAREHE**.11./.4../.2022



CS CamScanner